MWONGOZO WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAPORI YA AKIBA, MAPORI TENGEFU NA ARDHIOEVU WA MWAKA 2021

_____

SEHEMU YA KWANZA

1.1 Utangulizi:

Ibara ya 27(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inampa kila mtu wajibu wa kulinda maliasilia zote za nchi. Aidha, Ibara ya 9(c) ya Katiba inaruhusu rasilimali za nchi kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote. Kutokana na msingi huo wa kikatiba, Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 inalenga kuhakikisha kuwa kuna uhifadhi endelevu wa rasilimali za wanyamapori na ardhioevu. Katika kufikia lengo hilo, Sera inahimiza uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori bila kuathiri mazingira kwa madhumuni ya kukabiliana na umasikini. Katika kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Sera inasisitiza, pamoja na mambo mengine, kuongeza uzalishaji katika sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo uvuvi.

Kwa mujibu wa Sera ya Uvuvi ya mwaka 2016, ushirikishaji wa wananchi kwenye ulinzi wa rasilimali za uvuvi ni muhimu katika kukabiliana na uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira. Sera inatambua mchango wa Wizara yenye dhamana ya maliasili katika kuhakikisha kuwa uimarishaji wa mifumo ya matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi zilizopo katika hifadhi za wanyapori unashirikisha jamii za wavuvi zinazozunguka maeneo ya hifadhi.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya Na 5 ya mwaka 2009 inaainisha madhumuni ya Sheria hiyo kuwa ni pamoja na kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori yanayozingatia sheria. Kutokana na msingi huo wa kisheria, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori inaruhusu kufanyika kwa shughuli za uvuvi katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya ardhioevu kwa kibali cha maandishi cha Kamishna wa Uhifadhi. Vilevile, kifungu cha 8 cha Sheria hiyo ya Wanyamapori, inampa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa TAWA ambaye ni Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA (CC) kuandaa miongozo ambayo itaiwezesha TAWA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Pamoja na kuwepo kwa masharti yanayohusu kufanyika kwa shughuli za uvuvi katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori haikuwa na mwongozo mahsusi wa shughuli za uvuvi katika maeneo ya Mamlaka. Kutokana na hali hiyo, shughuli za uvuvi zimekuwa zikifanyika bila kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori ingawa kumekuwa na jitihada za kiutawala za kudhibiti na kusimamia shughuli hizo katika maeneo hayo. Kufanyika kwa shughuli hizo bila ya kuwepo kwa mwongozo mahsusi kumesababisha kuwepo kwa changamoto zinazoathiri uhifadhi wa wanyamapori na mazingira pamoja na kuikosesha Serikali mapato.

1.2 Madhumuni ya Mwongozo:

Mwongozo wa Shughuli za Uvuvi katika Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Ardhioevu wa mwaka 2021 unalenga kuweka utaratibu mahsusi wa usimamizi na uendeshaji wa shughuli za uvuvi katika maeneo hayo. Kimsingi, Mwongozo unaweka masharti yanayohakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zilizopo katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu zinatumiwa bila kuathiri misingi ya uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori.

Baadhi ya masuala ambayo yanawekewa masharti katika Mwongozo huu ni pamoja na utoaji wa vibali vya uvuvi, muda wa kuvua, zana na njia zinazoruhusiwa kutumika katika uvuvi na wajibu wa jumla wa mvuvi anayefanya shughuli zake katika eneo lililo chini ya Mamlaka. Vilevile, Mwongozo unaainisha tozo mbalimbali ambazo Mamlaka itatoza katika kusimamia shughuli za uvuvi katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu.

1.3 Walengwa wa Mwongozo:

Maudhui ya Mwongozo huu yanawalenga wadau wa uvuvi katika maeneo yanayozunguka mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu. Aidha, walengwa wengine wa Mwongozo huu ni pamoja na maafisa wanaoshughulika na uhifadhi, uvuvi pamoja na watafiti.

SEHEMU YA PILI

2.1 Mwongozo wa Shughuli za Uvuvi:

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, Mwongozo huu unakusudia kuainisha masharti ambayo yatazingatiwa na watu wanaokusudia kufanya shughuli za uvuvi katika maeneo yaliyo chini ya usimamizi wa Mamlaka. Masharti hayo ni:

2.1.1 Masharti ya Utoaji Kibali cha Uvuvi

(a) Mamlaka inaweza kutoa kibali cha kufanya shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya usimamizi wake endapo mwombaji wa kibali atakuwa na leseni ya uvuvi iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi, Sura ya 378;

(b) Kibali cha kufanya shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya Mamlaka kinaweza kutolewa kwa mkazi wa eneo husika tu na baada ya mwombaji kufanya yafuatayo:
   (i) kujaza Fomu ya Maombi ya Kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu. Fomu ya maombi ya kibali itatakiwa kujazwa kila baada ya miezi sita;
   (ii) kulipa ada ya fomu ya maombi ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu ambayo haitarudishwa;
   (iii) kudhaminiwa na Chama cha Ushirika cha Wavuvi katika eneo husika kilichosajiliwa;
   (iv) kulipa ada ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu; na
   (v) kuridhia kwamba TAWA haitakuwa na wajibu wowote kwa madhara yoyote yatakayompata akiwa katika eneo la hifadhi.

(c) Kibali cha Uvuvi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(d) Mamlaka haitatoa Kibali cha Uvuvi kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania;

(e) Mmiliki wa kibali cha uvuvi atatakiwa kuwa na kibali wakati wote anapokuwa katika eneo lililo chini ya Mamlaka.

2.1.2 Masharti ya Utoaji wa Vibali vya Vyombo vya Uvuvi

(a) Mamlaka inaweza kutoa kibali kwa chombo cha uvuvi kutumika katika shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya usimamizi wa Mamlaka endapo chombo hicho kitakuwa na:
   (i) urefu usiozidi mita 11;
   (ii) leseni ya kufanya shughuli za uvuvi iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi, Sura ya 378;

(b) Kibali cha chombo cha uvuvi kinachotumika kwa ajili ya shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya Mamlaka kinaweza kutolewa baada ya mwombaji wa kibali kufanya yafuatayo:

(i) kujaza Fomu Maombi ya Kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu. Fomu ya maombi ya kibali itatakiwa kujazwa kila baada ya miezi sita;
(ii) kulipa ada ya fomu ya maombi ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu;
(iii) kulipa ada ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu;

(c) Mtu mmoja hatoruhusiwa kumiliki zaidi ya chombo kimoja cha majini kinachotumika kwa shughuli za uvuvi katika eneo la Mamlaka;

(d) Chombo kimoja cha uvuvi hakitoruhusiwa kuwa na wavuvi zaidi ya wawili;

(e) Kibali cha chombo cha uvuvi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(f) Kibali cha Chombo cha Uvuvi kitatakiwa kuwemo ndani ya chombo wakati wote kitakapokuwa katika eneo la hifadhi;

(g) Kibali cha Chombo cha Uvuvi kitalipiwa kwa kila siku ambayo chombo kitaingia ndani ya hifadhi;

(h) Mamlaka haitatoa Kibali cha Chombo cha Uvuvi kinachomilikiwa na mtu ambaye si raia wa Tanzania.

2.1.3 Taratibu za Kuingia na kutoka katika Eneo la Hifadhi

(a) Mvuvi ataingia na kutoka eneo la hifadhi kupitia maeneo yalioanishwa;

(b) Mvuvi hataruhusiwa kuingia na kutoka katika eneo la hifadhi isipokuwa kupitia eneo lililoanishwa;

2.1.4 Msimu wa Uvuvi

(a) Shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya Mamlaka zitafanyika kwa kuzingatia msimu wa uvuvi utakaotangazwa na Mamlaka.

(b) Mtu yeyote hatoruhusiwa kufanya shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya Mamlaka nje ya muda ulioainishwa kuwa ni msimu wa uvuvi.

2.1.5 Muda wa Uvuvi

(c) Shughuli za uvuvi zitafanyika katika eneo la hifadhi kuanzia mawio hadi machweo ya kila siku iliyo katika msimu wa uvuvi;

(d) Mvuvi mwenye kibali ataruhusiwa kutega nyavu katika muda uliotajwa katika aya (a) ambazo zinaweza kuachwa katika eneo la maji baada ya muda huo;

(e) Mvuvi hatatakiwa kuwepo ndani ya eneo lililo chini ya Mamlaka baada ya machweo isipokuwa kwa kibali maalum cha Mamlaka.

2.1.6 Makambi ya Wavuvi

(a) Kikundi cha wavuvi kitakachopewa kibali maalum cha kuwa ndani ya eneo la Mamlaka baada ya machweo hakitaruhusiwa kujenga kambi ya kudumu katika eneo hilo;

(b) Kambi ya wavuvi itapaswa kuwa na maliwato ya muda iliyojengwa kwa kutumia nyasi, matete au makuti umbali wa mita 60 kutoka kwenye ukingo wa mto, ziwa au bwawa;

(c) Kambi ya wavuvi itajengwa katika eneo ambalo Mamlaka itaelekeza;

(d) Mvuvi mwenye kibali hataruhusiwa kutoka nje ya eneo la uvuvi kwa umbali wa kilomita 3 kutoka katika ukingo wa mto, ziwa au bwawa.

2.1.7 Zana za Uvuvi

Shughuli za uvuvi katika eneo lililo chini ya Mamlaka zitaendeshwa kwa kutumia zana zilizoanishwa katika leseni ya uvuvi.

2.1.8 Matumizi ya vyombo vyenye injini

(a) Uvuvi wa kutumia vyombo vya uvuvi vinavyotumia injini hautaruhusiwa katika eneo lililo chini ya usimamizi wa Mamlaka;

(b) Mamlaka inaweza kuruhusu matumizi ya vyombo vya uvuvi vyenye injini isiyozidi 40HP kwa idadi ambayo itaona inafaa kutumika katika eneo lililo chini ya Mamlaka kwa kibali maalum kitakachotolewa baada ya kulipa ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(c) Chombo cha uvuvi kinachotumika hakitaruhusiwa kuendeshwa kwa mwendo unaozidi *knots* 10.

2.1.9 Uegeshaji wa Vyombo vya Uvuvi

(a) Chombo cha uvuvi kilicho na kibali cha kufanya shughuli za uvuvi katika eneo la Mamlaka kitaruhusiwa kuegeshwa katika eneo hilo kwa kuzingatia yafuatayo:
    (i) kiwe kinatumika kwa shughuli za uvuvi;
    (ii) kisivujishe mafuta;

(b) haitaruhusiwa kuegesha chombo cha uvuvi katika eneo la hifadhi nje ya msimu wa uvuvi;

(c) Haitaruhusiwa kufanya matengenezo au ukarabati usio wa dharura wa chombo cha uvuvi katika eneo la hifadhi.

2.1.10 Biashara ya Mazao ya Majini

(a) Mtu yeyote hatoruhusiwa kuingia katika eneo lililo chini ya Mamlaka kwa madhumuni ya kununua mazao ya majini isipokuwa tu kama mtu huyo

atakuwa na kibali cha kuingia katika eneo la Mamlaka baada ya kulipa ada ya kuingia katika eneo la Mamlaka iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(b) Mamlaka itatoza ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili kwa kila gari litakaloingia katika eneo la Mamlaka kwa madhumuni ya kuchukua mazao ya majini yaliyovunwa katika eneo la hifadhi;

(c) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara ya aina yoyote isiyohusiana na mazao ya majini katika eneo la Mamlaka.

2.1.11 Mwendokasi wa vyombo vya moto

Chombo cha moto kitakachoruhusiwa kuingia katika eneo la hifadhi hakitaruhusiwa kutembea mwendokasi unaozidi kilomita 50 kwa saa.

Kila mvuvi mwenye kibali cha kuvua katika eneo lililo chini ya Mamlaka atakuwa na wajibu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zote zinazohusu usimamizi wa maeneo yaliyo chini ya Mamlaka na masuala ya uvuvi. Katika kutimiza wajibu huo, mvuvi atakuwa na wajibu wa:

2.1.12 Wajibu Mahsusi wa Mvuvi

(a) kutoingiza aina mpya ya viumbe wa majini katika eneo lililo chini ya Mamlaka;
(b) kutoingiza wanyama au ndege wafugwao katika eneo lililo chini ya Mamlaka;
(c) kutoingiza au kutotumia ndani ya eneo la Mamlaka vitu vya milipuko, sumu au kemikali ya aina yoyote;
(d) kutotumia zana au njia, haramu za uvuvi kama vile kokoro, vyandarua, kukausha maji au kuziba mto;
(e) kutokata kuni katika eneo lililo chini ya mamlaka;
(f) endapo atalazimika kukausha samaki katika eneo la mamlaka, atatakiwa kuingiza kuni kutoka nje ya eneo la mamlaka;
(g) kutoingiza baiskeli ndani ya eneo la Mamlaka;
(h) kutoingiza pikipiki ndani ya eneo la Mamlaka;
(i) kutega nyavu katika namna ambayo haitazuia kutumika kwa matumizi mengine eneo la maji lililo chini ya Mamlaka;
(j) kutovua viumbe wa majini wasioruhusiwa kuvuliwa kwa mujibu wa Sheria; na
(k) kutofanya uvuvi wa burudani (sport fishing);
(l) kutunza mazingira ya eneo la hifadhi;
(m) kutoharibu kwa namna yoyote uoto wa asili;
(n) kutoa taarifa kuhusu uhalifu wowote unotarajiwa kufanyika au ambao umefanyika katika eneo la hifadhi;
(o) kuwasilisha kwa Mamlaka takwimu za uvuvi zinazoainisha idadi ya samaki na mapato yaliyopatikana kutokana na samaki waliovuliwa katika eneo la Mamlaka.

2.1.12 Wajibu Mahsusi wa Mamlaka

(a) Mtumishi yeyote wa Mamlaka, wakati wa usimamizi wa muongozo huu ataongozwa na Sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma;
(b) Mtumishi yeyote wa Mamlaka, wakati wa usimamizi wa muongozo huu, hataruhusiwa kujihusisha na vitendo vyovyote vya unyanyasaji au uonevu

dhidi ya wavuvi ikiwemo kudai kupatiwa hisani yoyote kama vile kupatiwa samaki au mazao ya samaki kinyume na taratibu.

2.1.13 Utekelezaji wa Mwongozo:

(a) Utekelezaji wa Mwongozo huu utaanza baada ya kuidhinishwa na Kamishna wa Uhifadhi na kusambazwa kwa wadau katika tarehe itakayopangwa;

(b) Mtu aliyepewa kibali chini ya Mwongozo huu hataruhusiwa kuhamisha kibali hicho kwenda kwa mtu mwingine;

(c) Mtu yeyote atakayekiuka Mwongozo huu atafutiwa kibali kilichotolewa chini ya Mwongozo huu;

(d) Mtu atakayefutiwa kibali kilichotolewa chini ya Mwongozo huu hataruhusiwa kuomba kibali chochote kinachohusu shughuli za uvuvi hadi baada ya muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kufutiwa kibali.

SEHEMU YA TATU
HITIMISHO

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa rasilimali za majini zilizopo katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu zinatumika kwa manufaa ya wananchi bila kuathiri uhifadhi wa wanyamapori. Mwongozo huu unalenga kuimarisha uvunaji endelevu wa rasilimali hizo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Ni matumaini ya Mamlaka kuwa kila mdau anayehusika atazingatia Mwongozo huu katika shughuli za uvuvi zinazofanyika katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu. Kuzingatiwa kwa Mwongozo huu kunatarajiwa kuleta matokeo chanya katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka.

JEDWALI LA KWANZA

FOMU NA VIBALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UVUVI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

KITUO:……

SEHEMU A (Ijazwe na Mwombaji wa Kibali):

Jina:……

Namba ya Simu:……

Anwani ya Makazi:…….....

Namba ya Leseni ya Uvuvi:…….....

Mamlaka iliyotoa Leseni ya Uvuvi:……..

Tarehe ya kutolewa kwa Leseni ya Uvuvi:……

Tarehe ya kumalizika kwa muda wa Leseni ya Uvuvi:…….....

Saini:……..Tarehe:……

SEHEMU B (Ijazwe na Chama cha Ushirika cha Wavuvi):

Jina la Chama:……

Anwani ya Chama:……

Namba ya Usajili ya Chama:……...

Mamlaka iliyosajili Chama:……..

Maelezo ya Chama kuhusu mwombaji wa Kibali:

……..

……..

……..

Saini ya Katibu wa Chama:……..Tarehe:……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

PICHA

KIBALI CHA UVUVI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA

KITUO:…….

Kibali kimetolewa kwa……(Jina)

Namba ya Simu……

Anwani ya makazi…….....

Muda wa Kibali kuanzia…….hadi:……..

Kwa shughuli za uvuvi katika eneo la……...

Ada iliyolipwa…… Namba ya malipo……..

Namba ya risiti…… Tarehe ya malipo ……....

……. ……

Saini ya Mpewa Kibali Saini ya Mtoaji wa Kibali

Tarehe …… Tarehe……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA CHOMBO CHA UVUVI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA

KITUO:……

SEHEMU A (Ijazwe na Mwombaji wa Kibali):

Jina:……

Namba ya Simu:……

Anwani ya Makazi:…….....

Namba ya Leseni ya Chombo cha Uvuvi:…….....

Aina ya Chombo:……...

Mamlaka iliyotoa Leseni ya Chombo cha Uvuvi:……..

Tarehe ya kutolewa kwa Leseni ya Chombo cha Uvuvi:……

Tarehe ya kumalizika kwa muda wa Leseni ya Chombo cha Uvuvi:…….....

Saini:…….Tarehe:……

SEHEMU B (Ijazwe na Chama cha Ushirika cha Wavuvi):

Jina la Chama:……..

Anwani ya Chama:……

Namba ya Usajili ya Chama:……..

Mamlaka iliyosajili Chama:……..

Maelezo ya Chama kuhusu mwombaji wa Kibali:

……..

……..

……..

Saini ya Katibu wa Chama:……..Tarehe:……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

PICHA

KIBALI CHA CHOMBO CHA UVUVI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA

KITUO:……

Kibali kimetolewa kwa:…….(Jina la Chombo) kinachomilikiwa na:……..(Jina la Mmiliki)

Namba ya Simu……

Anwani ya makazi:…….....

Namba ya Leseni ya Chombo:……

Aina ya Chombo:……...

Muda wa Leseni ya Chombo kuanzia:……..hadi…….

Muda wa Kibali kuanzia:…….hadi:…….

Kwa shughuli za uvuvi katika eneo la :…….

……. ……

Saini ya Mpewa Kibali Saini ya Mtoaji wa Kibali

Tarehe ……. Tarehe……..

JEDWALI LA PILI

ADA MBALIMBALI

Na.	ADA		KIWANGO	
			GCAs (TZS)	GRs (TZS)
1.	Fomu ya Maombi ya Kibali cha Uvuvi		10000(miezi sita)	15000(miezi sita)
2.	Kibali cha Uvuvi		3000(siku)	5000(siku)
3.	Fomu ya Maombi ya Kibali cha Chombo cha Uvuvi		10000(miezi sita)	15000(miezi sita)
4.	Kibali cha Chombo cha Uvuvi		500/ Siku	2000/Siku
6.	Kibali cha kutumia chombo cha uvuvi kinachotumia injini	HP 5	5000/ Siku	10000/Siku
		HP 15	10000/ Siku	20000/Siku
		HP 25	20000/ Siku	30000/Siku
		HP 40	30000/ Siku	50000/Siku
7.	Kibali cha kuingia katika eneo la Hifadhi kwa madhumuni ya ununuzi wa mazao ya majini		2000/ Siku	4000/ Siku
10.	Kibali cha gari linaloingia katika eneo la Hifadhi kwa ajili ya kuchukua mazao ya majini:	Chini ya Tani 3	5000/kwa safari kwa siku	10000/kwa safari kwa siku
		Tani 3 hadi chini ya tani 7	10000/kwa safari kwa siku	20000/kwa safari kwa siku
		Tani 7 hadi 10	20000/kwa safari kwa siku	50,000/kwa safari kwa siku